**Mapambano Dhidi ya Ndoa za Utotoni ni Jukumu Letu Sote**

World Vision
TANZANIA



# Ulinzi na Usalama wa Mtoto ni JUKUMU LETU SOTE

“*Kila mtu miongoni mwetu na ampendeze jirani yake, apate wema, akajengwe*”

~ Warumi 15:2

## Utangulizi

Kitabu hiki kimeandaliwa na Shirika la World Vision Tanzania kwa ushirikiano na Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT) kwa ajili ya kuelimisha jamii juu ya haki, ustawi wa mtoto na wajibu wa mzazi/mlezi katika kumlea na kumlinda mtoto. Watoto wengi wanafanyiwa vitendo vya kikatili na unyanyaswaji na hivyo kusababisha kushindwa kufurahia utoto wao na kuwaletea madhara makubwa kiakili, kihisia na kimwili.

Hali hii isipokomeshwa itaendeleza mzunguko wa umaskini na ukatili katika jamii zetu. Wazazi/walezi, viongozi wa dini na jamii kwa ujumla wanatakiwa kushiriki kikamilifu katika kuwalinda watoto. Bwana Yesu katika kitabu cha Mathayo 19:14 alionesha umuhimu wa kuwalinda watoto akisema *"waacheni watoto wadogo waje kwangu msiwazuie kwa maana mfano wa hao, ufalme wa mbinguni ni wao"*. Tunaamini kuwa kitabu hiki kitachangia katika kuelimisha na kuhamasisha jamii juu ya ulinzi wa mtoto na kuchangia katika kutokomeza vitendo vya ukatili dhidi ya watoto. Kitabu hiki kimetumia rejea mbalimbali kutoka



katika Biblia Takatifu. Kwa ajili ya mafundisho kwa watoto, familia, waumini, viongozi wa dini na jamii kwa ujumla.

## Mtoto ni Nani?

Mtoto ni mtu yeyote mwenye umri wa chini ya miaka kumi na nane (18). Tafsiri hii imetokana na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto, Mkataba wa Afrika kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto, Sera ya Maendeleo ya Mtoto na Sheria ya Mtoto Na. 21 ya 2009. Katika umri huu mtoto anahitaji malezi bora ili aweze kuishi vizuri, kushirikishwa, kulindwa na kuendelezwa kiakili kwa ajili ya maisha yake ya baadae ya utu uzima. Katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati 6:6 *"Na maneno haya ninayokuamuru leo, yatakuwa katika moyo wako; nawe uwafundishe watoto wako kwa bidii, na kuyanena, uketipo katika nyumba yako, na utembeapo njiani, na ulalapo, na uondokapo"* kwa kusudi la kuwapatia malezi bora.

## Haki za Mtoto

Watoto wana haki za kipekee kwa sababu ya umri wao mdogo na hali yao ya utegemezi ambayo inaweza kuwafanya wadhulumiwe na kutendewa vitendo vibaya. Watoto wote wana haki sawa bila kujali jinsia, rangi, kabila, dini, hadhi au hali ya afya. Umoja wa Mataifa, Serikali, wazazi/walezi na jamii kwa ujumla wana wajibu wa kuhakikisha watoto wanapatiwa haki zao. Yesu hakutaka haki za watoto zidharauliwe, Mathayo 18:10b *"Angalieni msidharau mmojawapo wa wadogo hawa"* na katika Mathayo 18:3 anasema *"Na yeyote atakayempokea mtoto mmoja mfano wa huyu kwa jina langu, anipokea mimi"*. Yesu alionyesha utetezi wa haki za watoto nasisi tufuate kielelezo chake.

Haki za mtoto zimegawanyika katika makundi makuu manne (4) yafuatayo:

i. **Haki ya Kuishi: Inahusu kulinda na kuendeleza uhai wa mtoto ikiwepo:**

  - Kuzuia magonjwa na kupata huduma za matibabu,
  - Chanjo na kufuatilia ukuaji
  - Lishe bora
  - Mavazi yanayositiri
  - Makazi salama
  - Maji safi na salama
  - Usafi wa aina zote

ii. **Haki ya Kuendelezwa:** Mithali 22: 6 inasema *"mlee*





*mtoto katika njia impasayo nae hataiacha hata atakapokua mzee".* Maendeleo ya mtoto kiakili yanajumuisha:

- Elimu (rasmi na isiyo rasmi)
- Tamaduni, mila na desturi sahihi za jamii yake.
- Kiroho
- Vipaji

**iii. Haki ya kulindwa:** Kuhakikisha mtoto analindwa dhidi ya:-

- Unyanyasaji na ubaguzi
- Ukatili (kimwili, kingono na kihisia)
- Unyonywaji ikiwa ni pamoja na ajira za utotoni
- Ukeketaji, ndoa za utotoni na ukatili wa kijinsia
- Mazingira hatarishi
- Kutelekezwa au kuachwa bila mlezi

Biblia inaonyesha jinsi wazalisha wa kiebrania walivyowalinda watoto na kuwanusuru na kifo dhidi ya amri ya mfalme iliyotolewa kwao nyakati hizo, haya tunayasoma katika kitabu cha Kutoka1:15. Akasema, wakati muwazalishapo wanawake wa kiebrania na kuwaona wa katika kuzaa, ikiwa ni mtoto mwanamume, basi mwueni, bali ikiwa ni mtoto mwanamke, na aishi. Lakini wale wazalisha walikuwa wakimcha Mungu wasifanye kama walivyoamriwa na Mfalme wa Misri, lakini wakawahifadhi hai wale wanaume.

### iv. Haki ya kushiriki

Kundi hili linahakikisha kwamba watoto wanapatiwa nafasi ya kutoa mawazo na kwamba maoni yao yanazingatiwa hasa katika maamuzi yanayo athiri maisha yao. Mtoto anapaswa kushirikishwa katika ngazi zote kuanzia kwenye familia, jamii na taifa. Katika Biblia tunaona jinsi Yesu alivyopendezwa na sifa kutoka vinywa vya watoto wachanga na wanyonyao, haya tunayasoma katika Mathayo 21:15-16 *"Lakini wakuu wa makuhani an waandishi walipoyaona maajabu aliyoyafanya, na watoto waliopaza sauti zao hekaluni, wakisema, Hosana, Mwana wa Daudi! Walikasirika"*. Katika ushiriki huu wa watoto Yesu alitetea na kusimama upande wa watoto wala sio upande wa maoni ya viongozi wa dini.

## Wajibu wa wazazi/jamii katika kuhakikisha watoto wanapatiwa haki zao

Watoto ni Baraka, Zab: 127:3 *"Tazama wana ndio urithi wa BWANA, uzao wa tumbo ni thawabu."* Na katika Marko 10:13 Biblia inasema *"Basi wakamletea watoto wadogo ili awague"* jamii ina wajibu wa kuwapeleka watoto kwa Yesu katika nyanja zote za maisha, kielimu, kiroho, kijamii na kiuchumi. Hivyo basi, wazazi/walezi wana wajibu wa;-

1. Kuwahudumia watoto wao na kuhakikisha wanapata mahitaji yao ya msingi.
2. Kuhakikisha kwamba watoto wanalindwa dhidi ya magonjwa, wanapelekwa kwenye chanjo, wanapatiwa huduma za afya na lishe bora.
3. Kuwaandikisha shule, kufuatilia maendeleo yao shuleni na kuwapatia mahitaji yote ya shule.
4. Kushirikisha, kuongoza wanashirikishwa, kuongozwa na kuhakikisha watoto wanatimiza wajibu wao kikamilifu ikiwa ni pamoja na kufuata imani, tamaduni sahihi, kuzingatia masomo, kujilinda, kujifunza na kusaidia kazi za nyumbani zisizo athiri elimu, afya na zinazoendana na uwezo wa mtoto.
5. Kuwalinda watoto dhidi ya kunyanyaswa, unyonywaji, kutelekezwa, kufanyiwa ukatili na kuchukua hatua pale ambapo haki za mtoto zimevunjwa.
6. Kushirikiana na serikali na wadau wengine katika kuhakikisha huduma zinapatikana kwa viwango stahiki katika maeneo yao.



# MAENEO YA PROGRAMU NA WAJIBU WA MZAZI/MLEZI

## Kuimarisha uchumi wa kaya

Sekta hii inalenga kuhakikisha kwamba familia au kaya zinaweza kukidhi mahitaji yao wenyewe kiuchumi kupitia uzalishaji wenye faida wa kilimo, ufugaji na biashara. Mzazi/mlezi anawajibu wa kuhakikisha anakuza kipato na uzalishaji ili aweze kuhudumia familia yake kwa lishe bora, kusomesha watoto, kuhakikisha wanapata mahitaji yote ya msingi na kupunguza madhara kipindi cha majanga. Vikundi vya uzalishaji na kuweka na kukopa vinawajibu wa kuhamasisha jamii na hasa kaya za watoto waishio mazingira hatarishi kujiunga na kusaidia watoto hao kupata mahitaji na haki zao. Familia nyingi zenye kipato duni zinawaona watoto wa kike kama sehemu ya kipato na hivyo kuwaozesha wakiwa watoto ili wapate mali. Kila familia ni lazima iboreshe uchumi wa kaya yake ili kuweza kuwaendeleza watoto wao na kuvunja mzunguko wa umaskini. Katika injili ya Yohana 10: 10b Yesu anasema *"Mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele"* Hili neno TELE linabeba uzima katika nyanja zote za maisha.





## Afya, Lishe, Maji na Usafi wa Mazingira

Sekta hii inalenga katika kuboresha afya ya mama na mtoto, lishe, kupambana na magonjwa kama HIV, upatikanaji na matumizi ya maji safi na vyoo. Familia na jamii vina wajibu wa kuhakikisha afya zinaboreshwa na kulindwa.Watoto ni lazima walindwe dhidi ya mgonjwa kwa kupatiwa chanjo, kuzingatia kanuni za afya na lishe. Hii ni pamoja na kutumia nguvu ya sauti ya umma na utekelezaji (CVA), kuendeleza majadiliano kati ya mtoa huduma na mpokea huduma katika kuhakikisha upatikaji wa huduma za afya kwa viwango stahiki. Jamii ina wajibu wa kuboresha upatikanaji wa chakula kwa watoto walio katika mazingira hatarishi, kwa mfano kwa kuanzisha bustani au mashamba ya kijiji.

Biblia inaonyesha jinsi wanafunzi wa Yesu walivyotoa sauti zao wakati uhitaji wa chakula ulipotokea katika jamii. Haya tunayasoma katika kitabu cha Mathayo 14:17 *"Wakamwambia, hatuna kitu hapa ila mikate mitano na samaki wawili"*. Majadiliano haya baina ya Yesu na Wanafunzi wake yalipelekea kupata utatuzi wa tatizo wa uhaba wa chakula.

## Elimu

Lengo la sekta ya elimu ni kuboresha upatikanaji sawa wa elimu bora kwa wasichana na wavulana kwenye jamii zetu. Elimu ni haki ya kila mtoto bila kujali hadhi, hali ya afya kama ulemavu, jinsia, rangi au kabila. Wazazi/ walezi wanawajibu wa kuhakikisha watoto wa kike na wakiume wenye umri wa kwenda shule wanaandikishwa shule, wanasoma, wanafuatiliwa maendeleo yao na wanapatiwa mahitaji yote ya kielimu. Jamii pia inawajibu wa kuhakikisha elimu, mazingira ya kujifunza ni bora na wanachangia katika upatikanaji wa chakula shuleni. Jamii pia inawajibu wa kushiriki katika uendeshwaji wa shule na kushiriki na watoto wao katika shughuli mbalimbali za kielimu kama makambi ya kusoma. Walimu, wazazi na walezi wafuatilie na wahakikishe watoto wote wa kike na kiume wanalindwa na vitendo vyote vya ukatili hasa wakati wa usiku katika kipindi chote watoto watakapokuwa kambini.

Neno la Mungu katika kitabu cha Mithali 4:13 linasema *"Mkamate sana elimu, usimwache aende zake; Mshike, maana yeye ni uzima wako"*



## Malezi ya kiroho na ulinzi wa mtoto

Hii ni sekta mtambuka inayohakikisha watoto wanakuzwa kiimani na walindwa dhidi ya unyanyaswaji, kutelekewa, kunyonywa na kufanyiwa vitendo vya ukatili. Familia zina wajibu wa kulea watoto kiimani, kuwapeleka watoto katika nyumba za ibada na kuhakikisha wanalindwa. Ni wajibu wa jamii kuachana na mila potofu kama ukeketaji, ndoa za utotoni na ukatili wa kijinsia, mambo yanayo changia kukandamizwa, kunyanyaswa na kurudisha nyuma maendeleo ya mtoto.



Biblia inatufundisha jinsi alivyolindwa mama na umbu lake Musa walivyohatarisha maisha yao katika kumlinda MUSA baada ya kuzaliwa, tunasoma haya katika kitabu cha Kutoka 2:3 *"Na alipokuwa hawezi kumficha tena, akampatia kisafina cha manyasi akakipaka sifa na lami, akamtia mtoto ndani yake, akakiweka katika majani kando ya mto"*. Inaonyesha katika malezi ya Musa katika nyumba ya Farao mama yake aliwekeza vya kutosha Imani juu ya Mungu ambayo Musa hakuisahau na alivyokuwa mtu mzima alianza kutetea ndugu zake waebrania.

# KAMPENI YA KUPINGA NDOA ZA UTOTONI

Shirika la World Vision na Jumuiya ya Kikristo Tanzania linaungana na serikali na wadau wengine katika kupinga ndoa za utotoni. Ndoa za utotoni ni ndoa ambazo mtu mwenye umri wa chini ya miaka 18 anaolewa/oa, yaweza kuwa iwe imefungwa kidini, kimila au bomani. Mtu chini ya miaka 18, hajakua kiakili, kihisia na kimwili kuweza kubeba majukumu ya ndoa, uzazi na kutunza familia. Nchini Tanzania, takribani 31% ya watoto wa kike wameolewa wakiwa na umri wa chini ya miaka 18. Hii ni idadi kubwa na inapaswa kukomeshwa ili watoto wa kike walindwe na kuendelea sawa na watoto wa kiume. Ndoa za utotoni zinavunja haki za binadamu ambazo zinaelekeza kuwa "mtu ni lazima awe na umri wa mtu mzima pale anapoingia katika ndoa, kwa ridhaa yake".

Bibia katika kitabu cha Ruthu 1:12-13 kinatoa picha kwamba kuoa au kuolewa kunahitaji umri wa mtu mzima. *"Kama ningepata mtoto mume hata usiku huu, na kuzaa watoto wa kiume, je! Mngesubiri hata watakapokuwa watu wazima?".* Hii inaonyesha mtu anatakiwa awe mtu mzima ndipo aoe/aolewe. Kwa Tanzania mtu mzima anaanza akifika miaka 18.





## Mambo yanayochangia mimba za utotoni

- Kipato duni/umaskini wa familia
- Kutokuthaminiwa kwa mtoto wa kike
- Imani na mila potofu
- Ufahamu mdogo juu ya madhara ya ndoa za utotoni
- Ukosefu wa fursa za elimu, hasa sekondari
- Mtoto kukosa mwongozo na elimu ya afya na uzazi wakati wa kubalehe/ kupevuka
- Ajira za utotoni za kazi za majumbani kwa wasichana

## Madhara ya ndoa za utotoni

- Madhara kiafya na kihisia kwa mtoto kujihusiha na mambo ya ngono na uzazi.
- Madhara kwenye elimu na maendeleo ya mtoto wa kike kwa kuacha shule
- Inamweka mtoto katika hatari ya kufanyiwa ukatili wa kijinsia
- Inaathiri afya ya mama na mtoto sababu mwili unakuwa haujapevuka ipasavyo
- Inaongeza hatari ya kuambukizwa magonjwa ya zinaa kutokana na elimu ndogo na kutokuwa na mamlaka juu ya mwenzi na ndoa.
- Inaongeza idadi ya watoto wenye mimba hivyo kuwafanya kuishi kwenye

maisha duni na mazingira hatarishi.

- Mtoto anapata madhara ya kutengwa kutokana na umri wao hawako tayari kukabiliana na majukumu ya familia.
- Kuongeza idadi ya watu wasiokuwa na elimu na maarifa yanayoweza kuwatoa kwenye umaskini.

## Mwitikio wa Jamii

Hesabu 32:16-17... *"lakini sisi wenyewe tutakua tayari na silaha zetu... na watoto wetu watakua katika hiyo miji yenye maboma".*

Ukatili dhidi ya watoto una athari kubwa kwa maendeleo ya mtoto kihisia, kitabia, kimwili na unaharibu maendeleo yake ya kijamii maishani yake yote. Jamii yote ina jukumu la kuhakikisha kwamba watoto wanalindwa. Sheria ya mtoto inamtaka mtu yeyote mwenye sababu ya kuamini kuwa mtoto amefanyiwa ukatili na unyonyaji, kutoa taarifa juu ya jambo hilo. Zifuatazo ni hali zinazopaswa kutolewa taarifa mara moja:

a) Mtoto anateseka au yuko katika hatari ya kupata madhara makubwa kama vile kufanyiwa ukatili, ndoa za utotoni, ukeketaji, kubaguliwa au kutengwa

b) Mtoto kapotea, katelekezwa au kafukuzwa nyumbani

c) Mtoto anatumikishwa kwa ajira za kinyonyaji

d) Mzazi au mlezi mwenye dhamana ya kumlea mtoto anakataa au kupuuza kumpatia mtoto mahitaji ya msingi.

Mwanajamii anapaswa kutoa taarifa kwa wafuatao;

- Viongozi wa serikali wa eneo husika
- Timu za ulinzi na usalama wa mtoto na wanawake
- Afisa wa Ustawi wa Jamii
- Polisi: Dawati la Jinsia na Watoto
- Kituo cha Afya
- Mashirika yanayotetea haki za mtoto kama World Vision na Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT)
- Shirika linalotoa msaada wa kisheria

**Kumbuka:** Kesi zote za jinai zinapaswa kuripotiwa kwa Afisa wa Polisi aliyepo ndani ya eneo husika mara moja. Pale ambapo rufaa itakuwa imefanywa kwa watu walioorodheshwa hapo juu, mtu huyo atatoa taarifa kwa Afisa Ustawi wa Jamii wa kata au yule wa wilaya ndani ya masaa 24 kwa ajili ya kushughulikia kesi hiyo na kufanya taratibu za kisheria.

*"Sema kwa ajili ya wale wasioweza kujisemea, kwa ajili ya haki za wote walioachwa ukiwa."*

~ Mithali 13:8

World Vision
TANZANIA

**World Vision Tanzania (WVT) – Head Office**

Radio Tanzania Road, Off-Njiro Road, Block C,
Plot No. 181 Njiro,
P.O Box 6070, Arusha, Tanzania
Tel: +255-27 254-9252/253/254
Fax: +255-27-254-9259
Email: tanzania@wvi.org
Website: www.wvi.org/tanzania

World Vision Tanzania    wv_tanzania

**Christian Council of Tanzania (CCT)**

P.O Box 1454, Dodoma
Direct line: +255 26 232 4748
Office: +255 26 232 4445
Website: www.cct-tz.org

